

Maswali

1. Mbona Waisraeli walinung'unika?
2. Walikuwa wananung'unikia nani?
3. Nani alikumbuka vile Mungu alikuwa amewalinda?
4. Mungu alisema atawapa Waisraeli nini?
5. Nini ilitokea jioni?
6. Nini ilitokea asubuhi?
7. Mikate iliyotumwa na Mungu iliitwaje? Ilionja namna gani?
8. Nini ilifanyika kama wangeweka mana mpaka kesho yake.
9. Waliweka kiasi gani siku ya sita?
10. Walipoweka mana kwa siku ya sita usiku kucha iliharibika?
11. Nini ilikuwako wakati watu walienda kukusanya mana siku ya saba?

Majibu

1. Walinung'unika kwa sababu walikuwa na njaa.
2. Walinung'unikia Mungu.
3. Musa alikumbuka kwamba Mungu alikuwa amewalinda.
4. Mungu alisema atawapa mikate na nyama ya kukula.
5. Ndege wanono waitwao kware walikuja jioni.
6. Mikate ilikuja asubuhi.
7. Mikate iliitwa mana. Ilionja kama biskuti na asali.
8. Mana ingeoza na kunuka kama ingewekwa mpaka kesho yake.
9. Siku ya sita walisanya ya kutosha siku mbili.
10. Hapana. Mana haikuoza walipoweka usiku kucha siku ya sita.
11. Hakukuwa na mana ya kusanya siku ya saba.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



16 Chakula kutoka kwa Mungu

Marejeo

Kutoka 16:1 – 30

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu aliwapa watu wake chakula jangwani ingawaje walinun'unika.

Maneno maalum

- 16.1 Waisraeli + jangwani + sahahu ulinzi wa Mungu + njaa + nung'unika
- 16.2 Musa + kumbuka Mungu + jioni + kware + asubuhi + mana + mikate kutoka kwa Mungu
- 16.3 Mungu alisema + kusanya + kwa siku moja tu + baadhi ya watu + weka mana usiku kucha + yeyusha + mbaya
- 16.4 Mungu alisema + siku ya sita + kusanya ya siku mbili + pumzika siku ya saba + hakuna mana siku ya saba

16.1 Baada ya muda mrefu, Waisraeli walichoka kusafiri jangwani. Walisahahu maajabu yote yenye Mungu alifanya Misri na vile aliwasaidia kuvuka Bahari ya Shamu kwa nchi kavu. Walianza kufikiria ni nini watakula. Baadhi yao walisema, “Ingekuwa afadhali kama tungebaki Misri kwenye tulikuwa na nyama nyingi na mikate ya kukula. Tutakufa kwa njaa hapa jangwani.”


Wengi wao walisema kwamba wanatamani wangebaki Misri. Kulikuwa na chakula kingi kule Misri. Watakula nini hapo jangwani? Karibu kila mtu alianza kunung'unikia Musa. Musa aliudhika sana na hao watu kwa sababu ya kunung'unika juu ya Mungu.

16.2 Musa alikumbuka vile Mungu aliwaokoa kutoka kwa Wamisri tena vile aliwalinda. Musa alijua Mungu atawalinda na kuona kwamba wana chakula cha kuwatosha. Lakini wengi wao walikuwa wamesahahu.

Mungu aliambia Musa mpango aliokuwa nao wa kuwapa watu chakula. Mungu alisema kwamba atawapa Waisraeli nyama ya kukula usiku huo. Asubuhi yake Atawapa mikate ya kula. Wakiona nyama na mikate watajua kwamba Mungu ametuletea na anatumia.

Jioni ilipofika, Mungu alituma ndege wanono, wazito waitwao kware karibu na kambi yao. Waisraeli waliwaokota, wakapika na kwa hivyo wakawa na nyama ya kula.

Asubuhi iliyofuata, Waisraeli waliona umande kwa majani nje ya kambi yao. Jua lilipowaka na kukausha umande, watu waliona vitu vidogo vya theluji baridi au mawe makubwa ya mvua sakafuni. Waliuliza, “Nini hii?” kwa sababu hawakujua ilikuwa nini. Musa aliwambia kwamba ilikuwa ndiyo mikate yenye Mungu aliwaahidi. Iliitwa Mana. Ilionja kama biskuti na asali.



16.3 Mungu aliwambia, kila asubuhi wawe wakikusanya ya kuwatosha kwa siku mzima. Wasichukue saidi ya kuwatosha kwa sababu ikienda mpa kesho yake, ingeozwa. Baadhi yao hawakusikiliza Mungu. Waliweka mana zingine usiku kucha, kwa hivyo ilipofika kesho yake ilinuka vibaya na ilikuwa imeozwa. Musa aliudhika nao sana kwa kuweka mana na kukataa kufanya vile Mungu alisema.

16.4 Siku ya sita Mungu aliwambia wasanye mana mara mbili zaidi iwe ya siku mbili. Mungu hakutaka wafanye kazi siku ya saba. Siku ya saba ilikuwa siku ya mapumziko. Lazima wasisanye mana siku ya saba. Mungu aliwambia mana waliyokusanya ya siku ya saba haitaharibika. Ilikuwa nzuri tu kama ya siku zingine sita.

Watu wengine hawakusikiliza Mungu. Walidhani watakusanya tu ya siku moja ya sita. Halafu wataenda kuchukuwa ingine siku ya saba. Lakini walipoenda siku ya saba kuchukuwa, hakukuweko na mana. Hawakuwa wamesikia yenye Mungu aliwambia.

Mana haikuja siku ya saba ya mapumziko kwa sababu Mungu aliambia Musa, “Siku sita mtakusanya mana lakini siku ya saba iliyo siku ya kupumzika hakutakuwa na yoyote.”

Muda wote Waisraeli walipokuwa jangwani, Mungu aliwatumia mana ya kukula na hiyo ilikuwa kwa miaka arobaini.